HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI

ANNA MKAPA SEKONDARI,

S.L.P 8824,

MOSHI.

TAREHE……

Kumb Na AMMSS/J/……..

JINA LA MWANAFUNZI ……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ANNA MKAPA WILAYA YA MOSHI MANISPAA, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii **mwaka 2021.** Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021.** Fika shuleni siku hiyo bila kukosa. Aidha kutakuwa na kikao cha wazazi/walezi wa kidato cha kwanza tarehe…… **Siku ya ……**mzazi/mlezi fika bila kukosa.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE YA SHULE:

Sare ya shule hii ni mashati mawili meupe ya mikono mifupi na suruali mbili kwa wavulana na suruali ziwe na makunjo miwili na zisiwe nyembamba ziwe na inchi kumi na nane”18”upana wa chini.Rangi ya kitambaa cha surual kimeambatanishwa.Sare ya wasichana ni shati/blauzi mbili nyeupe za mikono mifup kwa wasiovaa ushungi,wale wanaovaa ushungi watashona shoti kanzu yenye mikono mirefu na ushungi mrefu na sketi mbili ndefu hadi kwenye kifundo cha miguu kwa wote.Wasichana hawaruhusiwi kushona suruali

NB: Mwanafunzi ambaye atakiuka masharti ya ushonaji wa sare hatapokelewa shuleni,kwani kabla ya kupokelewa atakaguliwa.

MAHITAJI YA SHULE

1. Fedha za chakula sh. 70,000/= ziwekwe kwenye akaunti ya ANNA MKAPA SEKONDARI namba 40302533188 NMB
2. Kila mwanafunzi aje na rimu moja (1) ya karatasi,Fagio moja (1) la chelewa na Jalada (Folder file) moja (1) kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu zake.
3. Kila mwanafunzi aje na daftari za masomo kumi na mbili (12) kalamu na mkebe wa hisabati.
4. Ni muhimu kwa Mzazi mwenye uwezo kumnunulia mwanafunzi kamusi ya Kiingereza “Dictionary ya Oxford”

1. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyolekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote ilitolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia,yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la kusimamia uendeshaji wa elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni lazima

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utazopewa

d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.

e) Kutunza usafi wa mwili na mavazi na mazingira ya shule.

f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

h) Kutunza mali za umma

2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi

b) Ubakaji

c) Uasherati,ushoga ama usagaji.

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kuberi na hata ugoro.

e) Kupigana au kupiga

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

g)Kudharau Bendera ya Taifa

h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba

i) Kuoa au kuolewa

j) Kutoa mimba

k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi

m) Kuwa na simu ya mkononi au laini ya simu

n) Kupatikana na silaha kama vile jambia,panga,kisu nk

Tahadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyazingatia kikamilifu

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

……

SINDATO C. SEIYA

MKUU WA SHULE

FOMU A

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI ANNA MKAPA
MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi…….……
(Majina matatu kwa herufi kubwa)

Jinsia: Mvulana/Msichana…….……..

Tarehe ya kuzaliwa…….……..

Kijiji …….. Kata ……..

Tarafa …….. Wilaya …….…..

Mkoa ……..

Dini…… Dhehebu…….

Namba ya Mtihani STD VII…… Mwaka……

Shule ya Msingi……..

Jina la Baba/Mlezi…….

Kazi yake ……..

Mahali anapoishi…….…

Kata …… Tarafa……..…….

Wilaya……

Majina mengine ya ndugu wanaohusika na malezi ya mwanafunzi (Ni hawa tu watakaoruhusiwa kuwasiliana na uongozi wa shule kuhusu malezi ya huyu mwanafunzi)

(a)Ndugu…….

S.L.P……

Kazi yake ……..

(b)Ndugu yake ……..

S.L.P……..

Kazi yake ……...

Maelekezo mengine yoyote ambayo yataweza kusaidia uongozi wa shule katika kumlea mwanafunzi huyu
…….....
.....

JINA _____ JINA _____

…….. ……..
SAHIHI YA MWANAFUNZI SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

FOMU B

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI ANNA MKAPA

Sanduku la posta 8824,
MOSHI,
……

MGANGA MKUU WA WILAYA
……
……
…….

YAH: OMBI LA KUPIMWA AFYA

Tafadhali mpime …… (Jina la mwanafunzi) ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Anna Mkapa kama anafaa kiafya kuendelea na masomo. Tafadhali mpime katika maeneo yafuatayo na kujaza matokeo yake katika fomu hii

A.HALI YA MWILI

a) Mapigo ya moyo……
b) Hemoglobin …….
c) Kundi la damu (Blood group)……
d) Mkojo……..
e) Choo (stool)……
f) Macho …….
g) Masikio ……..
h) Mimba ……
i) Matatizo mengine …….
j) Magonjwa ya Ngono (Aina)…….

B.Amewahi/hajawahi kuwa na magonjwa yafuatayo:

a) Asthma……..
b) Kifua kikuu……...
c) Blood pressure ……
d) Vidonda vya tumbo ……..
e) Ukoma ……..
f) Ugonjwa wa akili……
g) Ugonjwa mwingine wowote ambao haujatajwa hapa……..

MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by a medical officer. I have examined the above student and consider that He/she is physically fit/unfit as a student

……. ……

DATE SIGNATURE&OFFICIAL STAMP

DESIGNATION……